

Swali: Je ni kweli kwamba kiganja cha mkono wa kushoto au wa kulia kikiwasha basi ni ishara ya kupata pesa?

---

Jibu ni LA!.. hakuna uhusiano wowote kiganja kuwasha na fedha kumjia mtu. Labda kama mtu huyo ana pepo la utambuzi ndani yake..

Kama mtu ana pepo la utambuzi basi anaweza kuhisi kitu Fulani kikimjia, ikiwemo pesa kutoka katika chanzo kisicho cha kiMungu, au akahisi hatari kutoka katika upande wa maadui zake (*maana yake upande wa Mungu*), na ishara hizo anaweza kuzihisi kwa njia kama hizo za kuwashwa mkono, au kuwashwa sehemu nyingine ya mwili.

Lakini mtu mwenye Roho wa Mungu hisia zake zipo katika Neno la Mungu..Anaposoma Neno la Mungu na kudumu katika uwepo huo basi anaweza kuhisi Baraka zijazo, au hatari ijayo.

Kwamfano Neno hili katika biblia linaweza kukupa hisia za Baraka zijazo...

*Mithali 13:11 “Mali iliyopatikana kwa haraka itapunguka; Bali yeye achumaye kidogo kidogo atazidishiwa”.*

Mtu akilisoma hili Neno la kulishika, tayari atakuwa anajua ni nini kitafuta katika shughuli anayoifanya.. lakini si kukisikilizia kiganja kinasema nini!.. Na maneno mengine yote ya Mungu ni hivyo hivyo..

Hivyo kwa hitimisho ni kwamba, Elimu ya kusoma viungo vya mwili na kutabiri mambo yajayo ni elimu ya adui na ya kupotosha..

Lakini pia kumbuka si kila anayewashwa mkono basi ana pepo la utambuzi!.. La!, mkono unaweza kuwasha kwa sababu nyingine yoyote ya kibaolojia, na mtu asiwe na pepo!.. (*Hata hivyo asilimia kubwa ya wanaowashwa mikono hawana mapepo*). Hivyo kilicho kikubwa na cha msingi ni kudumu katika Neno la Mungu.

Bwana akubariki.

Je kuwashwa mkono ni ishara ya kupata pesa?

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP,  
jiunge na channel yetu kwa kubofya link  
hii >> [https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx  
10](https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10)

Maran atha!

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:  
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au  
Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

Mafundisho mengine:

**KUOTA UNAPEWA PESA, KUNA MAANISHA NINI?**

Pesa za bindoni ni nini?(Marko 6:8)

Je! fedha ni jawabu la mambo yote? (Mhubiri 10:19).

**MADHARA YA KUTAFUTA ISHARA.**

Je kuwashwa mkono ni ishara ya kupata pesa?

Biblia inaposema Yesu ameketi mkono wa kuume inamaana gani?

Rudi nyumbani

Share on:  
WhatsApp